



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBITI

TAARIFA KWA UMMA

KUANZA KWA MFUMO MPYA WA UKUSANYAJI MAPATO (TAUSI) BADALA YA MFUMO WA ZAMANI (LGRCIS)

HALMASHAURI INAPENDA KUWAJULISHA WANANCHI WOTE KUWA SERIKALI IMEFANYA MABADILIKO YA MFUMO WA KULIPIA MALIPO YA USHURU TOZO NA ADA MBALIMBALI KWENYE HALMASHAURI ZOTE NCHINI.

KUTOKANA NA MABADILIKO HAYA, MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBITI ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE KUWA MFUMO WA ZAMANI WA UKUSANYAJI MAPATO (LGRCIS) ULIOKUWA UKITUMIKA KWENYE HALMASHAURI UMEFUNGWA RASMI HIVYO MFUMO MPYA WA TAUSI UTAKUWA UKITUMIKA KWA AJILI YA UKUSANYAJI WA MAPATO YA HALMASHAURI.

KUFUATIA MABADILIKO HAYO; WANANCHI, WATEJA NA WADAU WOTE WENYE KUHITAJI HUDUMA YA KULIPA USHURU, TOZO NA ADA MBALIMBALI ZA HALMASHAURI KAMA VILE: KODI ZA VIBANDA; LESENI ZA BIASHARA; VILEO; USHURU WA HUDUMA; VIBALI VYA UJENZI; USHURU

WA MAZAO YA MISITU; LESENI ZA UVUVI PAMOJA NA TOZO MBALIMBALI ZINAZOTOZWA NA HALMASHAURI MNAELEKEZWA KUZINGATIA NA KUWA NA VITU VIFUATAVYO:

- 1. NAMBA YA KITAMBULISHO CHA TAIFA (NIDA);**
- 2. NAMBA YA SIMU ILIYOSAJILIWA KWA NA KITAMBULISHO CHA NIDA;**
- 3. NAMBA YA UTAMBULISHO WA MLIPAKODI (TIN)**
- 4. CHETI CHA UTHIBITISHO WA MLIPAKODI (TAX CLEARANCE CERTIFICATE);**
- 5. ANUANI YA BARUA PEPE (EMAIL ADDRESS);**
- 6. NYARAKA NYINGINEZO MUHIMU KULINGANA NA BIASHARA YAKO.**

HIVYO KILA MFANYABIASHARA ATATAKIWA KUJISAJILI KWENYE MFUMO WETU WA TAUSI (tausi.tamisemi.go.tz) HUKU AKIWA NA NYARAKA TAJWA HAPO JUU.

MUHIMU ZAIDI NI KUWA: MFUMO MPYA WA TAUSI UTAKUWEZESHA WEWE MFANYABIASHARA KUPATA HUDUMA MBALIMBALI NA KUFANYA MALIPO YA USHURU, TOZO NA ADA MBALIMBALI BILA KULAZIMIKA KWENDA KATIKA OFISI ZA HALMASHAURI YAANI UTaweza KUJIHUDUMIA MWENYEWWE KWA NJIA YA MTANDAO (SELF SERVICE).

MFUMO HUU NI BORA NA UNA MALENGO YA KUHAKIKISHA WATEJA HAWAPATI USUMBUFU WOWOTE KATIKA ULIPAJI WA USHURU, TOZO NA ADA MBALIMBALI ZA HUDUMA NA BIASHARA WANAZOZIFANYA KWENYE HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBITI.

**KWA MSAADA NA MAWASILIANO ZAIDI WASILIANA NA MAAFISA WETU
KWA SIMU NAMBA ZIFUATAZO 0687828186, 0692943382, 0657384720 NA
0692234880**

KARIBU TUKUHUDUMIE

IMETOLEWA NA;



**MOHAMED MAVURA
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBITI**